

# Aina za mkopo

## Karatasi la uhakika wa muongozo wa pesa zako

Kunazo aina nyingi tofauti za mikopo.

### Aina za mikopo

- ▶ Mkopo wa gari ni wa kununua gari mpya au iliyotumika – sio kwa matumizi mengine. – sio kwa kifaa kingine.
- ▶ Mkopo usiotozwa faida hukuwezesha wewe uchukue vifaa nyumbani kabla ya kuvilipia.
- ▶ Mkataba wa mteja hukuwezesha wewe kukopa kifaa (kwa mfano, komputa ya nyumbani au televisheni) kwa muda fulani uliodhibitishwa kwenye mkataba.
- ▶ Kadi ya mkopo ni ya kununua vitu (vifaa na huduma) hadi kwenye kiasi fulani. Kadi hii inapatikana kutoka mkopeshaji (credit provider).
- ▶ Mkopo wa Nyumba ni wa kuinunua nyumba – sio wa kununua kifaa kingine.
- ▶ Mkopo wa mshahara ni mkopo wa muda-mfupi, kwa kawaida huwa ni kwa wiki chache tu.
- ▶ Mkopo wa kibinafsi ni kwa kitu unachotaji au unachotaka, kama kununua gari au kwa matumizi wakati wa likizo.
- ▶ Kukodisha-ili-kununua ni pale unaponunua kifaa kwa kukodisha kifaa kwa kiasi cha muda wa wakati.
- ▶ Kadi za duka hutumiwa kwa kawaida kama kadi za mkopo (credit card) lakini kwa kawaida wewe utalipa faida ya juu zaidi.
- ▶ Mkopo wa kuimarisha ni pale unapoweka mikopo yako yote kwenye mkopo mmoja.

### Kumbuka

- ▶ Kunazo aina nyingi tofauti za mikopo.
- ▶ Gharama za mikopo huwa ni tofauti kulingana na aina ya mkopo.
- ▶ Mikopo tofauti hutumiwa kwa sababu tofauti.
- ▶ Tafuta mkopo ambao ni bora kwako.

### Wapi kupata maelezo zaidi

Kwa maelezo zaidi kuhusu aina tofauti za mikopo, tembelea MoneySmart, [www.moneysmart.gov.au](http://www.moneysmart.gov.au), au pigia simu 1300 300 630. Wewe waweza pia kupigia Afisa wa Huduma ya Maelezo ya Fedha kwenye 13 23 00 ambaye atakusaidia zaidi kwa kupangia matumizi yako ya mikopo.



### Indira apata Mpango wa Mkopo Usio Na Faida

Indira anaye mashine ya kuoshea nguo ambayo inavuja. Anamwita fundi wa kuirekebisha ambaye anamwambia kuwa mashine yake ni ya zamani sana na hawezi kuirekebisha, na anamshauri Indira kununua mashine mpya.

Indira ana wasiwasi kwani hana pesa za akiba za kutosha kuinunua mashine nyingine mpya, Indira anaenda kwenye benki yake ili kupata mkopo wa \$500 ili kuinunua mashine ya kuoshea nguo ambayo aliiona dukani.

Benki inamwambia Indira kuwa hawatampa mkopo kwa kiasi cha pesa hizo.

Indira anapiga simu kwa nyumba ya ushirika iliyo mtaani kwake na kuongea na Angela ambaye ni mfanyi kazi kuhusu shida yake.

Angela anamwambia Indira ampigie simu Eric, mfanyi kazi wa Jumuiya kuhusu mpango wa Mkopo Usio Na Faida, ambao pia unaitwa NILS. Eric anajua yote kuhusu NILS. Angela anampatia Indira nambari yake ya simu.

Indira anampigia simu Eric kuuliza lini ataweza kukutana naye ili aweze kujifunza zaidi kuhusu NILS. Eric anamuuliza Indira aje kumuona na amuletee kadi yake ya Centrelink.

Wakati Indira alipokutana na Eric alimweelezea kuwa NILS ni ya watu ambao wanapata malipo ya Centrelink na wanahitaji kuwa salama na kupata haki ya mkopo ambao wanaweza kutosheleza kulipia. Anasema kuwa NILS ni ya kununulia vifaa muhimu vya nyumbani kama vile mashine ya kuoshea nguo, komputa au fanicha. Kupata mkopo humaanisha kuwa Indira atalipa pesa hizo, lakini si lazima alipe faida.

Eric na Indira walisuluhisha kuwa Indira anaweza kutosheleza kulipa \$20 kila wiki mbili kwa miezi 12 months. Eric alipangia mkopo wa \$500 ili Indira aweze kununua mashine ya kuoshea nguo.

Indira ana furaha kwa sababu mashine yake mpya ya kuoshea nguo ni bora zaidi na anaweza kulipia ile \$500 ndani ya miezi 12 zifuatazo.

This page has been intentionally left blank.